

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: “**TUME**”
DODOMA
Namba ya Simu:0738166703
0733 005 974
e-mail: secretary@psc.go.tz
Website: www.psc.go.tz



TUME YA UTUMISHI WA UMMA,
JENGO LA CHIMWAGA,
S.L.P. 1074,
DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkutano wa Kwanza wa Tume ya Utumishi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 unatarajiwa kuanza siku ya Jumatatu tarehe 25 Oktoba 2021 na kumalizika tarehe 12 Novemba 2021 Jijini Dodoma. Mkutano huu utapokea, utajadili na kutolea uamuzi Rufaa na Malalamiko mbalimbali yaliyowasilishwa Tume na Watumishi wa Umma ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka zao za Nidhamu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa leo na Katibu wa Tume, Bw. Mathew M. Kirama, Mkutano huu utaongozwa na Mwenyekiti wa Tume Mheshimiwa Jaji Rufaa (Mst.) Dkt. Steven J. Bwana. Shughuli nyingine zitakazofanyika katika Mkutano huu ni Kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa Majukumu ya Tume na Mpango Mkakati wa Tume ya Utumishi wa Umma kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026.

Imetolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Tume ya Utumishi wa Umma
23 Oktoba, 2021